#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 15

Julai - Septemba 2024

**JAMBO LETU**



**Jacqueline Msuya**
*Mhariri*

**NDANI...**



**05**
**HESLB MARATHON YAZINDULIWA KUELEKEA MAADHIMISHO YA MIAKA 20**



**07**
**Jopiness:**
**Asante Serikali, kuniwezesha kuendelea na masomo**




# PROF. MKENDA AZINDUA 'HESLB APP'

Disemba 16, 2024, Dar es salaam

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amezindua mfumo wa huduma kidigitali unaofahamika kwa jina la 'HESLB APP' ili kurahisisha huduma za utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Hafla fupi ya Uzinduzi wa 'HESLB App' ilifanyika Jumatatu, Disemba 16, 2024 katika ofisi za HESLB jijini Dar es salaam na kushuhudiwa na wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi wa vyuo vikuu, maafisa mikopo wa vyuo vikuu na wanahabari kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Katika hotuba yake ya uzinduzi wa 'HESLB App', Prof Mkenda alisisitiza kuhusu dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita kuona kuwa mamlaka zote za serikali katika ngazi mbalimbali zinaongeza ubunifu na ufanisi katika kuwahudumia wananchi.

"Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha inaweka mazingira ya kutoa huduma bora na kwa urahisi kwa wananchi na hasa kwa kutumia mifumo ya kidigitali…", amesisitiza Prof. Mkenda.

Aidha, kuhusu upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu na kati, Prof. Mkenda amewasisitiza waombaji mikopo kuweka taarifa sahihi na kamilifu kwenye maombi yao ya mikopo ili kuthibitisha uhitaji wao waweze kunufaika na mikopo ya elimu kupitia HESLB.

Awali, akimkaribisha Prof. Mkenda, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga alisisitiza umuhimu wa 'HESLB App' na kuongeza kuwa elimu zaidi itolewe kwa wanafunzi na wanufaika wa mikopo ili waweze kuitumia vizuri 'App' hiyo na kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia ametoa wito kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo vyuoni na wanufaika wa mikopo waliohitimu vyuo, kujisajili na kuanza kupata huduma kwa urahisi kupitia 'HESLB App'.

"Kupitia HESLB App, wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na kati wanapata fursa ya kujisajili kwenye mfumo wa 'Digital Disbursement' maarufu DiDiS, unaowawezesha kupokea malipo yao kwa njia ya kidigitali kwa usahihi, urahisi, na haraka…" amefafanua Dkt. Kiwia.

'HESLB App' ni mfumo wa kidijitali unaotumia simu janja (Android na iOS) ambao umetengenezwa na wataalamu wa ndani wa kitengo cha TEHAMA cha HESLB, kwa ajili ya kurahisisha huduma za utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi hapa nchini ikiwa ni mwendelezo wa jitihada zinazofanywa na HESLB ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wateja wake.

# BI ZAYNAB KITIMA ATEULIWA KUWA MJUMBE WA BoD



Na Mwandishi Wetu

Rais wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) Bi Zaynab Kitima ameteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, uteuzi unaompa nafasi ya kuwakilisha maslahi ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Tanzania katika vikao vya juu vya maamuzi vya HESLB.

Uteuzi wa Bi. Zaynab Kitima umefanyika Novemba 20, 2024 na unatazamwa kama hatua inayolenga kuimarisha uwakilishi wa vijana na wanafunzi katika maamuzi yanayohusu mikopo na masuala mengine muhimu ya elimu ya juu nchini.

Kitima ambaye ni mwanafunzi wa shahada ya Umahiri katika Chuo Kikuu Mzumbe amejipambanua kama kiongozi mwenye dhamira ya dhati ya kutetea haki za wanafunzi, na uteuzi wake unatarajiwa kuleta mabadiliko chanya, hasa katika kuhakikisha kuwa changamoto zinazowakumba wanafunzi katika mchakato wa mikopo zinashughulikiwa kwa ufanisi zaidi.

Hatua hii ya uteuzi inaashiria dhamira ya dhati ya serikali ya kuhakikisha ushirikishwaji wa wanafunzi katika nafasi za uongozi na maamuzi ya kitaifa zinapewa kipaumbele na wanapata nafasi za kupaza sauti zao.

Sambamba na hilo, TAHLISO inatazama uteuzi huu kwa namna ya kipekee ambapo imani kubwa inalenga katika usimamizi wa wanafunzi kwenye maamuzi yanayohusu mikopo ya elimu ya juu, hasa katika maeneo ya sera, usawa, na upatikanaji wa huduma bora kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Tangu ameingia madarakani mwezi Aprili mwaka huu, rais Kitima ameonesha uongozi thabiti katika kushughulikia changamoto zinazowakabili wanafunzi wa elimu ya juu nchini. Uteuzi huu ni wa miaka miwili ikiwa ni sehemu ya juhudi za serikali kuhakikisha uwakilishi wa makundi mbalimbali katika bodi za maamuzi unafuatwa ili kuimarisha uwajibikaji na maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

**Heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya mwema.**

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Amani Kakana

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Ramadhan Namaru

**Designer**
Abdul K. Msangi
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# AHSANTE MH. DKT. SAMIA S. HASSAN Kwa zawadi ya Mwaka Mpya

Ndugu wasomaji wetu karibuni katika Toleo No.16 la Jarida la HESLB Yako ambalo huchapishwa kupitia njia ya mtandao mara moja kwa kila robo ya mwaka, likiwa limesheheni habari mbalimbali za HESLB pamoja na habari za wadau, lengo likiwa ni kuwaleta wadau wa elimu na kuwaunganisha na HESLB kuwa kiungo kimoja cha mawasiliano.

Tarehe 19 Disemba mwaka 2024, HESLB ilibuka mshindi wa tatu katika Usimamizi Bora wa Rasilimaliwatu katika kundi linalojumuisha Mamlaka za Serikali Kuu na Taasisi zote katika Utumishi wa Umma

Tuzo hiyo imetolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye Mkutano wa Wakuu wa Idara za Utawala na usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma uliofanyika Dodoma, Disemba 17-19,2024.

Mfululizo wa mafanikio haya ya HESLB ni kutokana na ufanisi wa utendaji kazi ndani ya Bodi sambamba na maboresho ya mifumo ya Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kila nyanja kuanzia utoaji na upokeaji wa taarifa za ndani, taarifa za wanufaika katika Uombaji na Utolewaji wa mikopo, Uchambuzi wa taarifa za wanafunzi pamoja na kutoa fedha za mikopo kwa ufanisi tangu mwaka 2004/2005 mpaka sasa.

Wito wangu kwa Watumishi wote wa HESLB ni kuongeza ubunifu na maarifa katika kujituma na bidii katika kazi ili kuhakikisha tunaendelea kufanya kazi kwa Weledi ili kuweza kufikia malengo ya kitaasisi kwa miaka inayoendelea.




> *Disemba 19 2024, HESLB ilibuka mshindi wa tatu katika Usimamizi Bora wa Rasilimaliwatu katika kundi linalojumuisha Mamlaka za Serikali Kuu na Taasisi zote katika Utumishi wa Umma*

**KONA YA WADAU**




# HESLB YAKUTANA NA MAAFISA MIKOPO VYUONI

Na Mwandishi Wetu

Menejimenti ya HESLB leo Jumatano, Oktoba 16, 2024 imekuwa na kikao kazi na Maafisa wanaosimamia ofisi za mikopo ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya kati zaidi ya 150 kilichoanza jijini Arusha ili kujadili masuala yaliyojitokeza mwaka wa masomo 2023/2024 na kujiandaa kwa mwaka mpya wa masomo 2024/2025 ulioanza mwezi huu wa Oktoba, 2024.

Kikao kazi hicho cha siku mbili kinachoendelea katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), kimefunguliwa rasmi na Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Charles Mkombachepa ambaye amemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Paul Makonda.

Awali, katika hotuba yake, Dkt. Mkombachepa amesifu jitihada za Serikali ya awamu ya sita kuhakikisha inatoa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wenye sifa ili waweze kufikia ndoto zao.

"Tuipongeze Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha ili kuwasomesha vijana wa kitanzania … nimeambiwa

mwaka huu kiasi cha TZS 787 bilioni kimetengwa kwa ajili ya kusomesha wanafunzi mwaka huu 2024/2025, kati yao zaidi ya 80,000 ni wa mwaka wa kwanza".

Licha ya kuzindua kikao kazi kati ya Menejimenti ya HESLB na Maafisa wanaosimamia ofisi za mikopo ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya kati, maafisa 25 wametunukiwa vyeti na ngao kwa kutambua utendaji wao uliojipambanua ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za wanafunzi kwa wakati zikiwemo hati za malipo ya ada.

Wadau wengine wanaoshiriki katika kikao kazi hicho kitakachohitimishwa kesho Oktoba 17, 2024 ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi Zanzibar (ZHESLB), viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi TAHLISO na taasisi za fedha.

Menejimenti ya HESLB imekuwa ikifanya vikao kazi na maafisa wanaosimamia ofisi za mikopo vyuo tangu serikali ilipoanzisha ofisi hizo mwaka 2011 ili kila mara kuhakikisha wanafunzi wanufaika wa mikopo ya elimu wanapata huduma stahiki.

> *"Tuipongeze Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha ili kuwasomesha vijana wa kitanzania … nimeambiwa mwaka huu kiasi cha TZS 787 bilioni kimetengwa kwa ajili ya kusomesha wanafunzi mwaka huu 2024/2025, kati yao zaidi ya 80,000 ni wa mwaka wa kwanza.*



# Prof. Mkenda

## TUNAWEKEZA KATIKA ELIMU

Na Mwandishi Wetu;

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amewataka wadau wa elimu kuiunga mkono Serikali kutekeleza mageuzi nchini ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika elimu na ujuzi inayolenga kuliwezesha taifa kuwa na rasilimaliwatu yenye umahiri katika sekta mbalimbali ili kuinua uchumi wa nchi.

Prof. Mkenda ameyasema hayo Novemba 14, 2024 jijini Dar es Salaam wakati wa kufunga Kongamano la Nne la Kimataifa kuhusu ubora wa Elimu Tanzania, ambapo amesisitiza ni vema watanzania kujikita na kufanya uwekezaji wa kutosha katika elimu kwa sababu nchi inahitaji rasilimaliwatu mahiri itakayochangia maendeleo ya taifa kwa ujumla.

"Ombi moja kwenu wadau wa elimu, tushirikiane kusimamia ajenda yetu … tusiondoke kwenye reli, tuwe na mwelekeo mmoja tuwekeze kwenye elimu ujuzi ili kuhakikisha watoto na vijana wetu wanapata elimu bora na ujuzi", alisema Prof. Mkenda.

Aidha, Prof. Mkenda amewaeleza wadau hao kuwa katika mfumo mpya, elimu ya lazima itakuwa ni miaka 10, ambapo baada ya elimu ya awali, mwanafunzi ataendelea na elimu ya msingi miaka sita na kisha elimu ya chini ya sekondari miaka minne. Aidha, elimu ya Sekondari ya juu itakuwa miaka miwili.

Kongamano hili la elimu linatoa fursa kwa HESLB kujitathmini na kuweka mikakati ya namna ya kuboresha utoaji na urejeshwaji wa mikopo kutokana na ongezeko la mwamko wa uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za awali ambalo linaashiria ongezeko la idadi kubwa ya wanafunzi watakaokwenda vyuo vya kati na elimu ya juu kwa miaka ijayo.

> Ombi moja kwenu wadau wa elimu, tushirikiane kusimamia ajenda yetu ... tusiondoke kwenye reli, tuwe na mwelekeo mmoja tuwekeze kwenye elimu ujuzi ili kuhakikisha watoto na vijana wetu wanapata elimu bora na ujuzi

# HESLB MARATHON YAZINDULIWA KUELEKEA MAADHIMISHO YA MIAKA 20

- **Kufanyika Dar Feb 15, 2025**
- **Rais SMZ kuongoza**




Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia leo (Ijumaa, Disemba 20, 2024) amezindua mbio za hisani kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa na imeandaa mikakati ya kuboresha utoaji wa huduma ikiwemo ushirikishwaji wa wanufaika wake.

Dkt.Kiwia amesema, mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Februari 15, 2025 katika Viwanja vya Farasi (Green Grounds) jijini Dar es salaam.

Mgeni rasmi wa mbio hizo zinazojulikana kama HESLB Marathon, atakuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Dkt. Kiwia amebainisha wazi kwamba, fedha zitakazokusanywa kupitia HESLB Marathon zitatumika kununulia vifaa vya maabara ya shule mbili za sekondari; moja ya Zanzibar na nyingine ya Tanzania Bara. Ameongeza pia kuwa kiasi kingine cha fedha kitatumika kuboresha kituo cha HESLB cha huduma za simu kwa wateja ( HESLB Customer Call Centre)

Bodi ya Mikopo ilianzishwa rasmi mwaka 2004 chini ya aliyekuwa Rais wa awamu ya Tatu Hayati Benjamin Mkapa na kuanza majukumu yake mwaka 2005 ambapo mpaka sasa imetoa kiasi cha shilingi Trilioni 8 kwa wanufaika zaidi ya laki nane.



**Novemba 13 - Tanga:** Kikosi cha Timu ya Mpira wa Pete cha HESLB kilichoshiriki kwenye mashindano ya SHIMMUTA jijini Tanga.



**Novemba 25, 2024 - Dar es Salaam:** Wageni kutoka HELSB Zambia walipotembelea ofisi inayopokea malalamiko ya HESLB, na kupata maelezo kutoka kwa Afisa Mawasiliano Mwandamizi, Bi. Eline Maronga (wa kwanza kushoto) kuhusu namna Mfumo wa malalamiko wa e-Mrejesho unavyofanya kazi.



**Disemba 7, 2024 - Dar es Salaam: Washiriki wa "UDSM Marathon" kutoka HESLB kwenye picha ya pamoja baada ya kukabidhiwa medali.**




**Disemba 16, 2024 - Dar es Salaam:** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi wa HESLB kutoka kitengo cha TEHAMA (waliosimama) kwenye uzinduzi wa HESLB App. Kulia kwa Waziri ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. Hamisi Dihenga na kushoto kwa Waziri ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia.



**Disemba 16, 2024 - Dar es Salaam**: Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekonolojia Prof. Adolf Mkenda (wa kwanza kushoto) alipofika katika ofisi za HESLB (EZO) kwa ajili ya uzinduzi wa HESLB App. Kushoto kwa Waziri Mkenda ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. Hamisi Dihenga na kushoto kwa Mwenyekiti ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia.



# Jopiness:

## Asante Serikali, kuniwezesha kuendelea na masomo

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Jopiness Johansen, mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Usimamizi wa Biashara (B.A in Business Administration) kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ameishukuru serikali kwa kumuwezesha kuendelea na masomo kupitia mkopo alioupata kwenye rufaa mwaka huu wa masomo wa 2024/2025.

Jopiness ni mtoto wa nne kuzaliwa kati ya watoto tisa kwenye familia yake. Binti huyu ni mwenyeji wa mkoa wa Kagera na alihitimu elimu ya msingi mwaka 2016 katika shule ya msingi ya Amani iliyopo Bukoba mjini.

Kwa upande wa sekondari, Jopiness alihitimu kidato cha nne katika shule ya Sekondari Kwauso iliyopo wilaya ya Bukoba vijijini mwaka 2020 na kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari ya Lukole iliyopo Ngara, ambapo alihitimu mwaka 2023 na kufanikiwa kujiunga na elimu ya Juu katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kilichopo Dar es Salaam.

Baba yake Jopiness ni mfanyabiashara mdogo anayeuza kwenye kibanda mahitaji madogo madogo ya nyumbani ili kuweza kuihudumia familia yake, wakati mama yake anajishughulisha zaidi na shughuli za nyumbani ikiwa ni pamoja na malezi ya watoto.

"Mwaka wa kwanza sikufanikiwa kupata mkopo lakini sikukata tamaa kwa kuwa nilipata maelezo kuwa naweza kuomba tena kwa mwaka unaofuata wa masomo na kufanikiwa kupangiwa mkopo...", anaelezea Jopiness.

Kuhusu namna alivyoweza kusoma bila mkopo mwaka wa kwanza, Jopineness anasema haikuwa rahisi lakini aliomba msaada kwa ndugu na jamaa waliomwezesha kulipa ada na kupata kiasi kidogo cha kujikimu kwa mwaka wake wa kwanza chuoni. "…Hali ya maisha ya wazazi wangu ni duni, hivyo ni ngumu kuweza kunisomesha na kuhudumia familia, hivyo niliomba ndugu na jamaa wakanisaidia kwa kunichangia na nikafanikiwa kumaliza mwaka wa kwanza bila mkopo..." anasimulia Jopiness.

Kuhusu malengo yake baada ya kuhitimu shahada yake ya Usimamizi wa Biashara, Jopiness anasema anapenda biashara na anatamani atakapohitimu ajiajiri kwa kuanza na biashara ndogo na atakapopata mtaji wa kutosha akuze biashara yake kwa kutanua wigo wa kuanzisha nyingine. "Napenda sana biashara, na malengo yangu nikishahitimu nifanye biashara ya kuuza nguo za wanawake na watoto, … na kama nitatapata mtaji mkubwa nitaanza kuuza samani za ndani…" anasema Jopiness.

"Naishukuru sana serikali kwa kuwa inatambua uhitaji wa watanzania wanaojiunga kwa masomo ngazi ya vyuo vikuu na kuwasaidia kupitia mikopo. Vilevile naiomba Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi na kuwawezesha wanafunzi wahitaji kama mimi kutimiza ndoto zetu kwa kuwapa mikopo ya kutosha ili wasipate changamoto wanapokuwa chuoni …'' anasisitiza Jopiness.

Serikali kupitia HESLB imekuwa ikiongeza bajeti kila mwaka ili kuhakikisha wanafunzi wahitaji wanaojiunga na vyuo vikuu nchini wanawezeshwa kusoma na kutimiza ndoto zao. Kwa mwaka huu wa masomo wa 2024/2025, serikali ilitenga kiasi cha TZS 787 bilioni kutoka TZS 731 bilioni zilizotengwa kwa mwaka 2023/2024 ili kuhakikisha wanafunzi wengi zaidi wanawezeshwa kusoma vyuo vikuu.

> *"Mwaka wa kwanza sikufanikiwa kupata mkopo lakini sikukata tamaa kwa kuwa nilipata maelezo kuwa naweza kuomba tena kwa mwaka unaofuata wa masomo na kufanikiwa kupangiwa mkopo...*

HESLB Yako
inatoa wito kwamba,
Iwapo unataarifa za mdaiwa
sugu ambaye hajaanza kurejesha
na anakipato, tuma taarifa zake
kwa barua pepe
**fichua@heslb.go.tz)**
ujumbe wa
**WhatsApp 0739-665533**
**Simu 0736-665533**
kuanzia saa
**2:00 asubuhi - 10:00 jioni**
**Jumatatu - Ijumaa.**



# Vigezo vya mikopo viangaliwe upya Prof. Chibunda

Novemba 13, 2024, SUA -Morogoro

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amesema ipo haja ya kufanyia utafiti vigezo vya kuwachuja waombaji mikopo ili kuwapata wanafunzi wahitaji halisi ambao hawawezi kumudu gharama za chuo bila kugharimiwa na serikali.

Prof. Chibunda ameyasema hayo Novemba 13, 2024 katika Kampasi Kuu ya Edward Moringe Sokoine (EMC) SUA mjini Morogoro wakati akiongea na mmoja wa Watumishi wa HESLB ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Maslahi ya Wanafunzi (SAC) chuoni hapo kuhusu hali ya mikopo kwa wanafunzi waliodahiliwa katika chuo hicho.

Akifafanua zaidi, Prof. Chibunda amesema wengi wa wanafunzi wanaodahiliwa chuoni hapo hasa katika programu za kilimo na sayansi ya wanyama wanatoka katika kaya za kipato cha chini sana ambazo haziwezi kumudu kwa kiasi kikubwa gharama za chuo.

"Ni aghalabu kukuta kijana anayetoka familia ya kipato cha juu anayeishi mjini kuomba udahili wa masomo ya kilimo… wengi wanatoka vijijini kwenye kaya za kipato cha chini", amesema Prof. Chibunda.

Makamu Mkuu huyo wa chuo hicho kilichojikita katika Kilimo na Mifugo amesema ipo haja ya kupitia upya vigezo vitakavyowezesha kuwachuja wanafunzi wahitaji ili wote wapangiwe mikopo kuweza kumudu gharama za chuo na kusoma kwa utulivu hadi kuhitimu.

Aidha, Prof. Chibunda aliongeza kuwa HESLB inapaswa kuweka mikakati ya kuwaelimisha wazazi na waombaji mikopo kuwa ni muhimu kujiandaa kwa fedha za kujikimu kwa walau majuma mawili baada ya vyuo kufunguliwa ili kumudu gharama za mahitaji muhimu wakati wakikamilisha usajili chuoni na kabla ya kupata fedha za mkopo.

"Baadhi ya Wazazi wa wanafunzi wanamudu gharama ndogo za nauli na Bima ya Afya lakini hawawezi kulipia hata mahitaji ya chakula wakati mwanafunzi akisubiri kukamilisha usajili hali inayosabisha wanafunzi waishi maisha magumu wakati wakisubiri kuingiziwa fedha za mikopo … wazazi wengi pia wanaamini mwanafunzi akishapangiwa mkopo atakuta fedha chuoni", amesema Prof. Chibunda.

Hadi Novemba 13, 2024 kati ya wanafunzi 6,700 waliodahiliwa SUA katika programu mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2024/2025, wanafunzi takriban 5,500 walikuwa wameshajisajili na kati yao wanafunzi 3,600 walikuwa wamepangiwa mikopo.

Kila mwaka HESLB hutoa elimu kwa waombaji mikopo watarajiwa na kutangaza mwongozo wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji ambao unaainisha sifa, vigezo na masharti kwa waombaji mikopo wenye sifa kwa mwaka husika kabla ya dirisha la maombi ya mikopo kufunguliwa.

> *"Ni aghalabu kukuta kijana anayetoka familia ya kipato cha juu anayeishi mjini kuomba udahili wa masomo ya kilimo… wengi wanatoka vijijini kwenye kaya za kipato cha chini*

# WASILIANA NASI;

## DODOMA
Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la
Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA
NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA
PSSSF Plaza, ghorofa
ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR
Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900,Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA
PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA
Jengo la CAG, Ghorofa ya
Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA
NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya tatu,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu
na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM
Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

**Heri ya Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya mwema.**